102/3
KISWAHILI
KARATASI YA 3
FASIHI
NOVEMBA 2020
MUDA: SAA 2½

MTIHANI WA DIRA 10: FASIHI
Hati ya Kuhitimu Kisomo cha Sekondari
KISWAHILI
Karatasi ya 3
FASIHI
Muda: Saa 2½

MAAGIZO

- Jibu maswali manne pekee.
- Swali la kwanza ni la lazima.
- Maswali hayo mengine matatu yachaguliwe kutoka sehemu nne zilizobaki; yaani: Hadithi fupi, Ushairi, riwaya na Fasihi Simulizi.
- Usijibu maswali mawili kutoka sehemu moja.
- Watahiniwa ni lazima wahakikishe kwamba kurasa zote za karatasi hii zimepigwa chapa sawasawa na kuwa maswali yote yamo.
- Majibu yaandikwe kwa lugha ya Kiswahili

SEHEMU YA A: TAMTHILIA
KIGOGO: PAULINE KEA
LAZIMA

1. Fafanua jinsi mwandishi wa tamthilia ya kigogo alivyofaulu kutumia mbinu zifuatazo za uandishi.
   a) Jazanda (alama 10)
   b) Majazi (alama 10)

SEHEMU YA B: RIWAYA

ASSUMPATA K. MATEI: CHOZI LA HERI

Jibu swali la 2 au 3

2)"Mwanangu, usimpake tope baba yako. Amekulea kwa miaka yote hii kama mwanawe, japo kwa kweli hakuzaa wewe."

(a) Eleza muktadha wa dondoo hili. (alama 4)

(b) Kwa kurejelea wahusika wengine wanne wa kike katika riwaya, thibitisha matatizo manne yaliyowakumba katika jamii (alama 16)

3)Ukiukaji wa haki za binadamu ni jambo la kawaida katika chozi la heri.

Jadili.(alama 20)

SEHEMU YA C : HADITHI FUPI

CHOKOCHO NA D. KAYANDA (WAH) : ***TUMBO LISILOSHIBA NA HADITHI NYINGINE***

Jibu swali la 4 au la 5.

4. "**Mapenzi Kifaurongo**"
   a) " Hadi sasa mimi ni kama rubani aliyeharibikiwa na ndege angani"
      Onyesha ukweli wa kauli hii ukirejelea hadithi nzima. (alama 10)

   "**Shibe Inatumaliza**"
   b) "Hatuwezi kumaliza kula. Kila leo tunakula . Hiki na kile…"
      Fafanua dhana ya ulaji kama inavyojitokeza kwenye hadithi hii. (alama 10)

5. " **Ndoto ya Mashaka**"
   Mwandishi wa hadithi hii anatupa taswira ya jamii iliyozongwa na masaibu yanayotamausha. Tetea ukweli wa kauli hii. (alama 20)

SEHEMU D: USHAIRI

6. Jibu swali la 6 au 7

Akili zangu
Zasimama ufuoni
Macho yake
Yakikagua bahari

Papa,mkali kama mauti
Anahangaisha samaki
Kwa ndaro na maringo
Daima akijigamba
Kwamba baharini
Haupo uwezo unaotisha
Wala tisho linalomweza
Wakati anaedelea kutiririka
Huku miongoni mwa samaki
Wingu zito huzuni
Lazidi uzani

Kama kwa sumaku
Samaki wanavutwa pamoja
Na nyuma ya ngao ya umoja
Wanaenda mwendo wa mbele
Wakiimba nyimbo zenye cheche

Kwa hasira zenye moto
Papa anaongeza ukali
Bali umati wa samaki
Haulegei muumano
Wala mwendo wa mbele
Kupungua kasi

Mashambulizi makali
Ewaa! Mashambulizi!
Kutoka pande milioni
Dhibi ya papa muuaji

Sasa baharini
Nyimbo za ufanisi
Zinapaa angani
Kama moshi wa unahi
Na kubusu masikio

Kama muziki wa nyonza.

Maswali

(a) Huu ni utungo wa aina gani? (alama 2)
(b) Kwa kutoa mifano fafanua sifa zinazoufanya utungo huu kuwa shairi. (alama 4)
(c) Eleza mawazo ya mshairi katika shairi hili (alama 5)
(d) Taja na ueleze mbinu tatu za kifasihi katika shairi hili (alama 6)
(e) Eleza maana ya maneno yafuatayo kulingana na shairi (alama 3)
   (i) Ndaro
   (ii) Cheche
   (iii) Nyonza

7. Soma shairi lifuatalo kisha ujibu maswali.

1. Haki ya mtu thawabu kuidai sitasita
   Hata 'nipatishe tabu muhali mimi kukita
   Kulitenda la wajibu liwe hai au mata
   Nitafanya majaribu na inapobidi matata
   Haki yangu 'taidai hata iwe ni kwa vita

2. Haki ya mtu u'ngwana siseme mimi nateta
   Sitaukiri ubwana na jeuri unoleta
   Na ikiwa ni kuwaana sitajali sitajuta
   Sikiri kuoneana na kupakana mafuta
   Haki yangu 'taidai hata iwe ni kwa vita

3. Haki ifukie chini ipige na kuibuta
   'Tumbukize baharini 'tazamia kuifwata
   Ukaificheje jangwani nitakwenda kuileta
   Itundike milimani nitawana kuileta
   Haki yangu 'taidai hata iwe ni kwa vita

4. Haki ijengee ngome izungushe na kata
   Na fususi isimame iwe inapitapita
   Tainuka nishikame haki yangu kukamata
   Sifa kubwa mwanamme kwenda huku wasota
   Haki yangu 'taidai hata iwe ni kwa vita

5. Uungwana siuuzi kwa njugu au kashata
   Ahadi za upuuzi na rai kuitaita
   Kwa kila alo maizi hawi mithili ya bata
   Tope yake makaazi na chakula cha kunata

Haki yangu ‘taidai hata iwe ni kwa vita

Maswali

a) Bainisha dhamira ya mshairi. (alama 2)
b) Eleza umuhimu wa mbinu zozote mbili ambazo mwandishi ametumia kutosheleza mahitaji ya kiarudhi. (alama 4)
c) Andika ubeti wa nne kwa lugha tutumbi. (alama 5)
d) Fafanua aina tatu za urudiaji zilizotumiwa katika shairi hili. (alama 3)
e) Ainisha shairi hili kwa kuzingatia vigezo vifuatavyo. (alama 2)
   (i) Idadi ya mishororo
   (ii) Mpangilio wa vina
f) Fafanua toni ya shairi hili. (alama 1)
g) Taja nafsi-neni katika shairi hili. (alama 1)
h) Tambua na ueleze maana ya mshororo ufuatao.
   Mleo wa ubeti wa mwisho. (alama 2)

SEHEMU YA E: FASIHI SIMULIZI

8. (a) Taja vipera vine vya utanzu wa semi na utoe mfano mmoja mmoja kwa kila kipera. (alama 8)

(b) Onyesha tamathali zilizotumiwa katika.
   (i) Jambo usilolijua ni kama usiku wa giza. (alama 2)
   (ii) Mgeni ni kuku mweupe. (alama 2)
   (iii) Hawi Musa kwa kuchukua fimbo. (alama 2)
   (iv) Kiburi si uungwana. (alama 2)

(c) Fafanua nahau zifuatazo. (alama 4)
   (i) Ana jicho la nje.
   (ii) Yeye ni jamvi la wageni.
   (iii) Mkono birika
   (iv) Mfua uji.

MWONGOZO SHILINGI 65/ KWA 0707311302